https://dspace.org/

# Ushairi Wa Kisufi Katika Tendi Za Kale Za Kiswahili: Mfano Wa Utendi Wa Siri Li Asrari

**Karama, Mohamed; Chimerah, Rocha; Wa Mutiso, Kineene**

**2018-03**
The Africa Premier Research Publishing Hub
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/414

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

Mara Research Journal of Kiswahili
Vol. 3, No. 1, March 2018, Pages 1 – 9, ISSN 2520-0577

# USHAIRI WA KISUFI KATIKA TENDI ZA KALE ZA KISWAHILI: MFANO WA UTENDI WA SIRI LI ASRARI

Mohamed Karama*[1] Rocha Chimerah[1] Kineene wa Mutiso[2]
[1]Idara ya Kiswahili, Pwani University
[2]Idara ya Kiswahili, University of Nairobi
Email: ifarymrca09@gmail.com

* Corresponding author

Received: February 26, 2018
Published: March 12, 2018

**Ikisiri**

Usufi ni njia mojawapo ya kumuabudu Mungu katika dini ya Kiislamu. Kuna tariqa kadhaa za kisufi katika Afrika Mashariki na zote zina lengo moja kuu la kumpwekesha Mungu. Nyingi ya tendi za kale za Kiswahili, haswa za kabla ya Karne ya Ishirini, zina maudhui kuhusu dini ya Kiislamu. Makala haya yanaangaza kuhusu njia hii ya kumpwekesha Mungu kwa kutumia ushairi wa tendi ili kufikiliza ujumbe huu wa kisufi. Nadharia ya Usemezano inashikilia kwamba maana haswa ya neno hupatikana kwa kuangalia muktadha wa maneno yalipo(vyo)tumika katika kauli nzima. Kwa kutumia msingi huu wa kuchunguza muktadha tutathibitisha kauli yetu kwamba tendi za kale za Kiswahili zina athari ya kisufi na katika Utendi wa Siri li Asrari ndipo tutakapochukua data yetu. Tumesampulisha itikadi, daraja, na lugha ya kisufi inavyojidhihirisha kwenye utendi huu na kutoa uchanganuzi wa kimaelezo. Tunahitimisha kwamba usufi umemwathiri kwa kiwango kikubwa mtunzi wa utendi huu na lengo lake na la kisufi ni moja – kumpwekesha Mungu.

**Maneno Muhimu:** Usufi, Siri li Asrari, Usemezano, Uislamu, Fasihi.

© 2016 by the author(s); Mara Research Journals (Nairobi, Kenya) **OPEN ACCESS**

## 1. Utangulizi

Makala haya yamelenga kuonesha ushairi wa kisufi katika *Utendi wa Siri li Asrari*, mpaka hivi sasa, utendi wa zamani zaidi unaojulikana katika fasihi ya Kiswahili uliyotungwa na Mwanamwarabu binti Bwanalemba (au, Mwanalemba). Mkabala huu wa kisufi ndani ya *Utendi wa Siri li Asrari* ni kadhia ambayo bado haijashughulikiwa na ndiyo sababu moja ya makala haya. Usufi ni njia fulani ya kumuomba Mungu na ushairi wake umejiweka tafauti kadamnasi ya ushairi wa aina nyingine. Matumizi ya maneno katika ushairi wa kisufi yana lengo na shabaha yake ni kumtukuza Mungu, kwa hivyo, tamathali zote za usemi zinazotumiwa katika shairi la kisufi ni kumlekeza binadamu amuabudu na kumpenda Mungu tu. Madhumuni ya makala haya ni kuonesha namna maneno yanayotumika katika *Utendi wa Siri li Asrari* (soma *Siri*) yanavyotupeleka kumjua Mungu na kumtegemea Yeye katika majambo yetu yote.

Makala haya yataangaza juu ya maana ya usufi, sifa za masufi, daraja zao, na hatimaye, lugha ya ushairi wa kisufi ndani ya *Siri*. Katika kuujua usufi ndiyo itatupa ufunuo wa kuelewa matumizi ya misamiati ainati iliyotumika ndani ya *Siri* na sanaa za lugha zilizomo humo. Makala haya yatajikita katika *Siri* peke yake kama kiwakilishi cha kuonesha na kuthibitisha ushairi huu wa kisufi katika mashairi ya kikale ya Kiswahili. Makala haya hayatojishughulisha na historia ya usufi au tariqa (njia) za kisufi zilizoko katika ulimwengu wa Kiislamu kwa ujumla na, kwa uchache, Afrika Mashariki.

Bakhtin anashikilia kwamba maana ya maneno haiwezi kujulikana bila ya kuangalia muktadha wa mahali na wakati lilipotumika (Holquist, 1981). Kulingana na Baldick (2001:50) anaeleza 'muktadha' kuwa ni, 'maelezo ya kijamii, kitamaduni, kihistoria au ya kiwasifu kuhusu neno fulani na mahali lilipotumika neno hilo kati ya maneno mengine kwenye matini'. Tukitaka kuyafahamu maneno yaliyotumiwa na mtunzi wa kazi ya *Siri* ni lazima tuangaliye muktadha yalipo(vyo)tumiwa maneno hayo. Bakhtin anasema kuangalia maneno kikamusi hayaleti maana *haswa* iliyotarajiwa badala yake yanaleta maana ya *kijuujuu* na hapo maana haswa itakuwa bado haijajulikana (keshatajwa hapo juu (khj)). Kwetu sisi kuyafahamu maneno yalivyotumiwa katika *Siri* tumeyanasibisha na ufuasi wa kisufi wa dini ya Kiislamu. Makala haya yatathibitisha kwamba tukitumia mwelekeo huu wa muktadha wa kisufi maneno mengi yaliyotumika ndani ya *Siri* yataeleweka kwa ufasaha zaidi.

Mapitiyo yetu kuhusu utendi huu yanaonesha kwamba bado haujashughulikia kadhia hii ya kisufi, bali pia utendi wenyewe haujashughulikiwa vilivyo kiuhakiki. Kazi kadhaa zimeweza kutueleza jambo kuhusu utendi huu, walakini, lengo la kazi zao lilikuwa tafauti na lengo letu la kudhihirisha usufi katika *Siri*. Mutiso (1996) alishughulikia *Kasida ya Burudai* na kuonesha aina za motifu zilizomo ndani ya kasida hiyo na humo imetajwa motifu ya hirizi na hivyo kurejelea *Siri* kwamba wahusu hirizi pia. Wesah (2005) amekwenda zaidi katika uchambuzi wake na kuchanganua tendi mbili ukiwamo wa *Siri* kuhusiana na mbinu za lugha zilizotumika humo. Lakini naye hakushughulikia kadhia hii yetu ya usufi katika *Siri*. Knappert (1979) ameutaja utendi huu kwa ufupi na kipande kikubwa hakukitaja katika kazi hii wala hakushughulikia usufi katika *Siri*. Dammann (1940) na Mutiso (2003) wamefanya kazi ya kuuhifadhi utendi huu kwa khati za Kilatini na pia kuutafsiri kwa Kijarumani na Kingereza mtawalia, lakini hawakutowa maelezo kuhusu usufi kama tutakavyofanya sisi katika makala haya.

### *2. Siri* kwa Ufupi

*Siri* umetungwa na Mwanalemba karibu karne tatu unusu zilizopita na una beti 563. Mwanzo wa utendi wazungumzia vita anavyopigana Mtume Muhammad (nabii wa waislamu) dhidi ya Andharuni ambaye anasawiriwa kuwa adui wa waislamu. Vita vikali vinapiganwa na Andharuni, katika awali ya vita, anashinda. Andharuni anaonesha ujabari na nguvu zisizo za kibinadamu namna anavyopigana. Mtume Muhammad anaomba nusura kwa Mola wake, ambaye mtunzi anatuonesha kwamba ndiye mtegemewa katika majambo yoyote na yote humu ulimwenguni. Mtume Muhammad anaitikiwa dua yake ya kupata wokofu dhidi ya adui Andharuni kwa kuambiwa kwamba Andharuni ana hirizi kichwani mwake ndiyo inayompa nguvu hizo za kiajabu. Mtume Muhammad anaipata hirizi hiyo, kwa msaada wa ndege aliyetumwa na Mungu kuishopowa kichwani, na baada ya muda anamshinda Andharuni. Katika sehemu ya pili ya utendi huu, Mtume Muhammad anakuja kuelezewa na Mwalimu Jibril (malaika mtukufu) faida ya hirizi hiyo ambayo ni ya majina matukufu ya Mwenyezi Mungu. Mwandishi anatuusiya sisi wasikilizaji/wasomaji wa utendi huu tushikamane na hirizi hiyo ya majina ya Mungu ili itufaidi hapa duniani na kesho akhera.

### 3. Usufi wa Kiislamu ni Nini?

Kwa maelezo ya Lings (1975:41) na Schimmel (1975:14), akimrejelea Hujwiri, neno 'sufi' lina maana ya 'mteule na Mungu', mtu anayevaa nguo za sufi, au, watu walioko mstari wa mbele katika kumuomba Mungu. Pia laweza kumaanisha mtu nadhifu (msafi). Wote wanakubaliana kwamba wakati wa Mtume Muhammad neno hili halikuwako hata baada ya kidogo kufariki dunia Mtume Muhammad. Walikuja kujulikana kwa jina hili watu hawa kwa sababu ya namna walivyokuwa wakimuabudu Mungu sana mpaka yote yaliyoko ulimwenguni hayana maana kwao bali walitaka kukutana na Mola wao tu.

Kulingana na Lings (1975:17) anasema kwamba usufi wote ulimwenguni ni sawa kwa sababu masufi wote wanalenga kwenye kumtafuta Mungu wa Kweli. Lakini, kitu kinachoutafautisha usufi wa Kiislamu kimeelezwa na *Kuruani* (kitabu kitakatifu cha waislamu tafsiri ya Barwani (1995)) kwamba, '...ni kumuamini Mungu, na Mitume Wake, na Vitabu Vyake (*Zaburi, Taurati, Injili, na Kuruani*) na Malaika

Wake.' Al Haddad (2003:136) anasema kwamba ukishapiga Shahada kwamba umekubali Mungu ni mmoja na Mtume Muhammad ni mtume wake basi kazi iliyobaki ni kuamini kwamba Yeye na mitume wake na vitabu (miongozo) vyake na malaika wake wapo na Yeye Pekee ndiye mtendesha mambo katika ulimwengu huu na Mungu haulizwi namna anavyoyaendesha hayo mambo.

Sheikh Abdulkadir Jelani (1992), al Haddad (2003), Lings (1975), na Schimmel (1975) wote wanaonesha kwamba baada ya kukiri kwamba Mungu ni Mmoja Pekee na kuamini kuwa Mitume na Vitabu na Malaika na majaaliwa yanavyotokea basi muumini amefikia kiwango kinachoitwa *Ihsan*. Hii ndiyo daraja ya juu kabisa ya kuamini. Muumini akifika daraja hii basi kila kitu chake ni Mungu: kula kwake, kulala kwake, kuinuka kwake, kutembea kwake, kusoma na hata kuvuta pumzi kwake ni Mungu tu – haoni kitu kingine ila Mungu tu. Kulingana na *Kuruani* si wengi katika binadamu wanaofikiya daraja hii, ni wachache sana, na Yeye Mungu peke yake ndiye anayewajua mawalii wake.

Mtunzi wa *Siri* anatuonesha itikadi hii ya kisufi anaposema:

201. Kwa rehemayo, Karimu
Turahamusi kaumu
Urahamuo dawamu
Wajao twise simazi!

208. Kula yambo mpulike
Li katika dhati yake
Kutekeleza ni kwake
Moliwa wetu Azizi.

319. Ya Rabbi anta arhamu
Fa ma lahum Maula
Ghairuka ya Rabbi.

326. Kutekeleza ni kwake
Mkuu wa ezi ni yake
Allahumma ni ye pweke
Aso shirika wa ezi.

Katika beti hizi mtunzi anatuonesha kwamba kila kitu kinakwenda kwa matakwa ya Mungu na apendavyo Yeye. Ndio mtunzi akasema kila kitu kiko katika dhati yake (ubeti wa 208). Mwisho, katika ubeti wa 319 akatuonyesha kwamba Mtume Muhammad anakubali waja wake hawana Mola mwengine isipokuwa Yeye. Malaika Jibrili (ubeti wa 326) ndiye anayetuonesha kwamba Mungu ni Allah pekee na hana mshirika katika anayoyafanya.

Lakini yote tuliyotaja hivi sasa kuhusu kushikanisha shahada, iman, na ihsan ni njia kuu ya kumpwekesha Mola, kilele chake ni kutufikisha kwenye *la ilaha illa Allah* 'hapana Mola ila Allah' (Lings, 1975:21) na al Haddad (2003:37) akaongeza 'Muhammad ni Mtume wa Allah'; shahada mbili ambazo hazitenganiki wakati wa kukiri Uola. Maneno haya ya *la ilaha illa Allah* ambayo Sheikh Abdulqadir Jelani (1992) anasema hakuna mfano wake. Kulingana na masufi ni lazima muumini aseme Mungu Mmoja Pekee kwa sababu hivyo Mungu anakuwa hana mwenginewe na kwamba hagawanyiki baina ya Mungu na Kiumbe (Lings, 1975:65). Ndio Mtume Muhammad akashurutizwa aseme, 'Sema! Mungu ni Mmoja Pekee' katika *Kuruani* (112:1) na sura hii ikaitwa 'Ikhlas' kwa maana ya 'uthabiti wa kauli' kwamba ni Yeye tu na hakuna mwengine mfano wake.

Tangu mwanzo wa utendi huu, mtunzi amerejelea kauli hii 'hapana Mola ila Wewe' katika ubeti wa 6 hadi wa 9 na kwingi ndani ya utendi. Walakini wakati anapomaliza utendi wake mtunzi anamaliza kwa kauli hii ya *la ilaha illa Allah*. Anasema:

563. La Ilaha ila llahu
La Ilaha ila llahu
La Ilaha ila llahu
Pweke Mola Muawazi.

Mtunzi amerudia maneno ya *la ilaha illa Allah* mara tatu katika mishororo mitatu ili kuleta ikirari kwamba anakubali na kujinasibisha na maneno hayo. Maneno hayo yana maana ya 'hapana Mola isipokuwa Mungu' yenye kumpwekesha Mungu. Kisufi haya ndio maneno anayojifunga nayo sufi katika maisha yake yote na atakapoondoka ulimwengu huu, sufi anataka yawe maneno yake ya mwisho kutamka ndio aingie katika radhi ya Mungu na natija yake ni kupata pepo. Na mtunzi ndivyo alivyofanya katika utendi wake ubeti wa mwisho ni kauli hii ya shahada.

Utendi wenyewe unaisha kwa tarakimu ya witri ambayo haigawanyiki mara mbili. Ubeti wa mwisho una tarakimu ya 563 na haigawiki mara mbili sawasawa. Hii ni sifa ya kisufi yenye kumfanya Mungu hata katika tarakimu ukigawanya witri lazima itabakia moja; na moja ni Mungu hagawiki uwili wala hana mshirika. Sifa hii ya witri ndiyo apendayo Mungu mwenyewe kwa sababu huonesha upekee wake, kama alivyosema Mtume Muhammad kwamba Mungu ni witri apenda mambo kiwitri. Jambo hili la witri limebainika kwenye idadi ya beti za utendi huu.

### 4. Daraja za Masufi

Tumesema hapo juu kwamba usufi ni kumpwekesha Mungu pekee katika ibada zako zote wewe muumini. Kuwa sufi kuna misukosuko mengi na awezaye kuipita na kufikia kumkurubia Mwenyezi Mungu basi sufi huyo huwa amefikia kiwango kikubwa sana (Lings khj.). Wengi kati ya wanaojaribu kufikia daraja ya sufi hushindwa njiani kutokana na majaribu wanayopawa na Mungu na wachache wanaobaki huitwa *walii*, yaani mcha Mungu sana. Katika *Siri* neno hili limetumiwa kwa watu wawili pekee: Mtume Muhammad na Ali. Watu hawa wawili wanaaminiwa na mtunzi kwamba wamefikia daraja hii ndipo aliposema:

198. Uso wakwe mcha Mungu
Kekeza yiu la mbingu
Kamba, 'ewe Moli wangu,
Nijazi, Rabi, nijazi!'

176. Kamwamkuwa Aliyi
Bunu Abi Talibiyi
Karama llahu takiyi
Wajahahu kana mwezi.

Mtunzi amemtaja Mtume Muhammad katika mshororo wa kwanza ubeti wa 198 kuwa 'mcha Mungu' na Ali katika ubeti wa 176 mshororo wa tatu kwa neno 'takiyi' lenye maana ya 'mcha Mungu'. Watu hawa wawili inaaminika katika dini ya Uislamu wako katika daraja ya juu ya kumuogopa Mungu na ndio maana mtunzi hakuacha kuwapa heshima yao katika utendi.

Katika *Kuruani* (56:7-9) Mungu anatoa daraja hizi za masufi na wasiokuwa masufi. Kuna *mukarrabun* (waliyo karibu na Mungu). Wenye sifa hii ya 'karibu na Mungu' ni kina Abubakar, Umar, Uthman, Ali na mkewe bibi Fatma, na Hassan na Hussein, na mtunzi amewataja katika beti za 13 hadi 16. Kuna na *as-habul yamiin* (watu wa mkono wa kulia) na *as-habu shimali* (watu wa mkono wa kushoto). Kwenye kundi

hili la ‘watu wa mkono wa kulia’ ndio tunawapata sahaba zake Mtume Muhammad na ndio hao aliyowataja mtunzi kutoka ubeti za 88 hadi 99. Watu wa mkono wa kulia, mbali ya Mtume Muhammad na sahaba zake tuliyowataja, pia wamo waumini waliomfuata Mtume Muhammad kama alivyosema mtunzi katika ubeti wa 17. Kundi la watu wa mkono wa kushoto, ambao ni watu wa kwenda motoni kwa vitendo vyao viovu, wanajumuisha Andharuni na kundi lake lote. Mtunzi anasema:

19. Na hao makufari
Walaniwa kwa umuri
Makazi yao ni nari
Hawatoshusha pumzi.

41. Kala shehe amenena
Na huyu Andharuna
Ni kafiri maluuna
Upotevu ndio kazi.

Katika beti hizi mbili tunapata kujua ni kwa nini watu hawa wa mkono wa kushoto wamo katika kundi hili. Kazi yao kubwa ni kufanya ubaya na kupoteza watu na kwa sababu ya hivyo, basi mwisho wao ni kutiwa motoni. Katika utendi huu tofauti hizi za watu zinajitokeza na hivyo kutusaidia kuelewa dhamira ya mwandishi kuweka wahusika wake katika makundi. Kundi la watu wa tabaka la juu katika ucha Mungu halafu walioko mkono wa kumeni na walioko mkono wa kushotoni. Kwa hivyo, mgawanyo huu wa wahusika umewekwa kutokana na kigezo cha kiusufi – nani anayemuogopa Mungu sana – anayemuogopa Mungu sana ndiye mtakatifu na asiyemuogopa Mungu ni muovu.

### 5. Ushairi wa Kisufi katika *Siri*

Baada ya kujua sifa na daraja za masufi sasa tutachanganua namna usufi unavyojitokeza katika lugha ya *Siri* na namna tutakavyofunukiwa kuuelewa utendi huu.

### 5.1 Kuanza na Jina la Mungu

Sifa hii ya kuanza na jina la Mungu katika utendi ni sifa inayodhihirika katika tendi nyingi za Kiswahili kwa mfano *Al Inkishafi, Mwanakupona* (katika Shitemi (2010). Kwa hivyo, mtunzi wa *Siri* naye hakuiepuka sifa hii. Tangu mwanzo wa utendi mtunzi anajikurubisha na Mola ili aweze kumsaidia katika utunzi wa utendi huu. Huku kutaka ilhamu ya Mola wakati wa kutunga kazi ya fasihi limo hata katika fasihi za jumuia nyingine ulimwenguni, kwa mfano, Kiyunani (Butcher, 1922). Kuna imani kwamba uongozi wa Mungu katika jambo lolote halina budi kuwa zuri tena ni lenye kufaulu – kwa sababu Yeye ndiye mtendesha mambo, kama wanavyoamini masufi na mtunzi huyu hakuepuka ada hiyo. Kwa mfano, matumizi ya maneno ‘*bismillahi*’ (ubeti 3), ‘*rahimani*’ na ‘*rahimi*’ (beti 4 na 5) mtawaliya. Kutajwa kwa Mtume Muhammad na maswahaba wake pamoja na dhuria yake katika (beti 10 - 16); maombi yanayofanywa na Mtume wakati wa vita (ubeti 158) kumuomba Allah; majina ya Sayyidna Ali (ubeti 238); na maelezo yote anayopewa Mtume Muhammad na mwalimu Jibrili ni kuonesha kwamba utendi huu umeelemea Usufi.

Bismillahi Rahmani Rahiim
Wa bihi nastaiinu.

3. Nowe ina la Wadudi
*Bismilla* nibutadi
Ndiye pweke wa abadi

Mfalume mwenye ezi.

4. Ndiye pweke *Rahimani*
Muawazi duniani
Wema na wawi yuwani
Atateuwa Azizi.

5. Na *al Rahimi* tataya
Sifa za Mola Jaliya
Mtukufu wa wilaya
Wahidu Llahu Muyuzi.(msisitizo ni wetu)

Katika beti hizi tunaona mtunzi akijitegemeza kwa Mungu ili amsaidiye katika utunzi wa kazi hii. Anasema, 'Bismillahi Rahmani Rahiim Wa bihi nastaiinu' maana yake, 'naanza kwa jina la Mungu na kwake yeye twaomba msaada'. Kwa hivyo, anatanguliza jina la Mola na kumsifu kwamba yeye ndiye anayesaidia watu katika majambo yao. Katika beti za 3-5 mtunzi anayataja majina matukufu ya Mungu (herufi za mlazo) ili kujiegemeza na Mungu katika kadhia yake na ndivyo wafanyavyo masufi kama tulivyotaja huko nyuma (kumtegemea Mungu kwa kila kitu).

### 5.2 Vita baina ya Haki na Batili

Katika sehemu ya mwanzo wa utendi huu kuna vita vinavyotokea baina ya waislamu wakiongozwa na Mtume Muhammad na wasiokuwa waislamu wakiongozwa na Andharuni. Nguli wa *Siri* ni Mtume Muhammad (ubeti 85) na nduli wa vita hivi ni Andharuni (ubeti 27).Vita hivi tunaviona ni baina ya haki ikiendelezwa na wachaji Mungu na batili ikiendelezwa na wanaomkufuru (wanaompinga) Mungu. Vita hivi vimeletwa makusudi na mtunzi kuonesha kuwa wachaji Mungu kila siku ndiyo watakaofaulu pindi wanapomtegemea Mungu. Katika vita hivi Mtume Muhammad alistaajabu namna Andharuni anavyowapiga waislamu. Mtume Muhammad akaomba apawe nusura ili aweze kumshinda Andharuni. Lakini hata Mtume Muhammad alipopawa hirizi hiyo yenye nguvu haikumfaidi kumpiga Andharuni kwani bado aliendelea kushindwa. Ndiyo akaomba tena kwa Mungu mbona hashindi na hirizi anayo yeye basi Mungu akamfungulia kwamba lazima amtegemee Yeye Mungu Pekee na wala sio kitu chingine chochote. Alipofanya hivyo Mtume Muhammad alimshinda Andharuni.

### 5.3 Hirizi na Uwezo Wake

Matumizi ya istiara ya 'hirizi' na taharuki bila kufichua hiyo 'siri ya masiri' hadi mwishoni mwa utendi pamoja na matumizi ya chuku kuhusu uwezo wa hirizi hiyo ni katika kutuonesha kuwa mtunzi amemiliki usanifu wa lugha na ni mkwasi wa misamiati na istilahi zinazofungamana na ushairi wa kisufi.

25.Tena ina manufaa
Mtu atakaoivaa
Humwepukiya baa
Na zitimbi za gharazi.

Katika ubeti huu tunaelezewa umuhimu wa hirizi hiyo ambayo utakapoivaa basi hutopata balaa yoyote. Hirizi hii ina nguvu kushinda nguvu yoyote nyingine wakati wa kufanya kwake kazi. Mtunzi anatwambia hivi:

442.Ewe Mtume Mmaka
Lau uyapotamka

Ukaomba kwa Rabuka
Kwa dua hinu Azizi.

443. Ukaomba kwa Jalali
Kondoka kuu jabali
Katika yo majabali
Yalo bora mafumizi.

444. Lingaliondoka upesi
Kwa amri ya Mkwasi
Na jamii ya unasi
Wakilandika maozi.

Katika beti hizi Mtume Muhammad anaambiwa akiomba kwa hirizi hii basi lau ataka majabali na milima iondoke yote ingefanyika tena na huku yuwaona ikifanyika. Lakini ni mwisho wa utendi huu ndipo mtunzi anapotufungulia kwamba si hirizi kijaluba na ndonga kuvaliwa shingoni bali ni jina tukufu la Mungu. Alitumia taharuki ya hali juu kuficha ufumbuzi wa 'siri ya masiri' mpaka mwisho ndipo anapotufumbulia. Mtunzi anatoboa siri hivi:

531. Hirizi hinu tukufu
Ni maina ya Latwifu
Yuwa ewe msharafu
Muhamadi msikizi.

Katika ubeti huu Mtume Muhammad anaambiwa kwamba hirizi iliyokuwa ikitajwa tangu mwanzo wa utendi ni hirizi ya majina matukufu ya Mwenyezi Mungu. Na majina hayo kulingana na Mtume Muhammad ni 99 na moja ndilo tukufu zaidi Mwenyezi Mungu amelibana na anataka waja wake walitafute kwa kumuomba Yeye. Wanaokuja kulijua jina hilo ni masufi, wachaji Mungu peke yao, na ni wachache sana. Kwa hivyo masufi wanaregeshwa palepale kwa Mwenyezi Mungu na hawategemei chochote chingine.

### 5.4 Masufi na *Skaz*

Katika utendi huu kuna matumizi ya *skaz*, lugha ya kikawaida aliyoielezea Bakhtin (Holquist, 1981). *Skaz* ni aina ya lugha inayotumiwa na watu wa kawaida katika miktadha ya pasipo sheria wala vikwazo vya kuzungumza (Schmid, 2013). Utendi huu umejitoa na kuwa tafauti na tendi nyingine za kisufi kutokana na matumizi ya maneno 'machafu'. Matumizi ya 'mbwa' (ubeti 71) kumaanisha matusi, 'kafiri' (ubeti 54), 'mnwa shizi' yaani mlevi (ubeti 53), 'kafiri mwizi' (ubeti 32) ni baadhi ya maneno ambayo tendi nyengine kufu yake *Siri* kama *Al Inkishafi, Mwanakupona* (katika Shitemi (2010)) na *Hamziya* (Mutiso, 2005) hamna maneno 'makali' yasiyotumia tasfida katika kutamkwa kwake.

32. Yanenewa pakhubiri
Ya kwamba tumwa bashiri
Alisikia habari
Ya huyu *kafiri mwizi*.

53. Kwa ubora wa husuni
Kuritifai yangani
Ikatisha mashetwani
Na jamii *wanwa shizi*.

54. Na hoyo *mbwa kafiri*
Andharuni jairi
Naye asitaakhari
Mambo kitengeza kozi.

71. Na ndani mwa kitambaa
Cha hoyo *mbwa* juhaa
Asodhuru, asofaa
Mtokozwa ni Azizi. (Msisitizo ni wetu)

Matumizi ya maneno 'mbwa', 'kafiri', 'mwizi', 'wanwa shizi' (mlevi) ni maneno ya matusi yenye ukali fulani aliyoyatumia mtunzi katika utendi huu. Ni maneno ya kutukana waziwazi bila tasfida yoyote. Maneno haya yanatuarifu juu ya Andharuni, nduli wa Mtume Muhammad na kiwakilishi cha mhusika muovu katika utendi huu.

Nilipotembelea tovuti ya sufi (http://sufism.org/writingsonsufism tarehe 26/3/2017) pameelezwa humo kwamba muumini akishafikia kiwango cha juu cha usufi mambo yote kwake ni mazuri hakuna ubaya hata Schimmel (1982:9) ameonesha kwamba mpaka baina ya uzuri na ubaya pengine haupo. Uzuri unatokana na Mungu na ubaya pia unatokana na Mungu kwa sababu Yeye ndiye muumba wa kila kitu (Schimmel, 1975:198). Walakini al Haddad (2003:49) na Ibn Taymiyah (2000:178) wamepinga hatua hii ya kumtusi mtu 'kafiri' au neno lolote baya kama 'mbwa'. Kwa sababu mcha Mungu wa sufi kikweli huchunga ulimi wake kwani Mtume Muhammad amekataza kumwita mwislamu au hata mtu mwengine 'kafiri'.

Nafsi iliyoumbwa na Mungu imepewa majivuno ndio inayompelekea binadamu kuasi na kufuata matamanio na kumsahau Mungu na sufi anatahadharishwa na kufuata matamanio ya nafsi, yanayopoteza. Binadamu anapofuata nafsi huwa amemuweka Mungu kando na sasa amechagua mshirika mwengine katika kutendesha mambo (Lings, 1975). Kwa sababu ya kutafautisha baina ya Mungu na kiumbe kingine, mtunzi wa *Siri* anapiga kelele na kutukana kwa lugha ambayo watu wa kawaida wataiona ni matusi, ilhali kwa sufi lugha hii ni waadhi kwa mtu aliyechagua mungu mwengine kumtumikia na kumuacha Allah.

Sababu ya pili ya kutumia aina hii ya lugha, ni kwamba masufi walitaka kufikisha ujumbe wa dini na mapenzi yao ya Mtume Muhammad kwa kutumia lugha ya kawaida, lugha ya ummah. Lugha ya mazingira inayofahamika na wengi na wala sio lugha za kiteule ambazo haziwahusu watu wa kawaida (Schimmel, 1982:137). Schimmel anasema kwamba ushairi wa kisufi ulianza kama lugha ya kidini lakini baadaye lugha isiyo ya kidini iliingia katika ushairi huu. Tukiuangalia kwa mtazamo huu, tutafahamu na kuelewa kwamba mtunzi alitumia lugha hii ya kawaida katika ushairi kuhusu dini ili kuvunja fikra ya uteule katika dini (khj.:139). Mtunzi wa *Siri* alikuwa ameshavuka maisha haya ya kawaida na yuko katika maisha ya daraja ya juu ya kisufi, ndiposa akatumia lugha hii 'chafu' ambayo kwake yeye ni makemeo na namna ya kuonyesha njia ya salama na ya amani na kufaulu maisha haya ya duniani na ya kesho akhera ambako ndiko kila sufi anapopania kupafika.

## 6. Hitimisho

Makala haya yametowa maelezo kuhusu maana ya usufi na namna unavyojidhihirisha katika Uislamu. Pia yameonyesha kwamba katika usufi kuna daraja za usufi na masufi huwekwa katika matabaka kutokana na uwezo wao wa kuumcha (kumfuata) Mwenyezi Mungu sana. Pia tumeonesha namna usufi unavyojitokeza katika *Siri* na kutoa beti zinazoweka wazi ithibati hii. Makala haya pia yamejadili na yamethibitisha kwamba lugha ya masufi inatakiwa iwe safi kama lilivyo jina lao. Lakini, kupitia lugha ya kikawaida ya watu wa kawaida wasiyochunga sheria za uzungumzi, maneno 'machafu' yaliyotumika katika utendi huu si

machafu bali ni mazuri kwa sababu ya kumrudisha binadamu kumuabudu Mungu na kuwacha kudanganyika kufuata Mola mwingine. Hatimaye, tumetimiza lengo letu kuu la kuonesha kwamba usufi unapatikana katika tendi za kale za Kiswahili kwa mkabala wa *Utendi wa Siri li Asrari*.

### 7. Marejeleo


Baldick, C. (2001). *The concise Oxford dictionary of literary terms*. New York: Oxfrod University Press.

Barwani, A. M. (1995). *Tarjama ya al muntakhab katika tafsiri ya Qur'ani tukufu*. Beirut: Dar ul Fajri Islamy.

Butcher, S. H. (mh.).(1922). *The poetics of Aristotle*. London: Macmillan &Company Limited.

Dammann, P.E. (1940). *Dichtungen in der Lamu mundart des Suaheli* Band 28. Hamburg: Freiderichesen.

Emerson, C., & Holquist, M. (wah.). (1986). *Speech genres and other late essays.*Austin: The University of Texas Press.

Haddad, A. M. (2003). *Key to the garden*. London: Starlatch Press.

Holquist, M. (mh.). (1981). *M. M. Bakhtin: The dialogic imagination*. Austin: The University of Texas Press.

Jelani, M. A. (1992). *The secret of secrets*. Cambridge: Islamic Texts Society.

Knappert, J. (1979). *Myths and legends of the Swahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Lings, M. (1975). *What is sufism?* Lahore: Suhail Academy.

Mutiso, K. (1996). *Archetypal motifs in Swahili Poetry: Kasida ya burudai*. Tasnifu Shahada ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Mutiso, K. (2003). *Utenzi wa siri li asirali* [afuan] *with a translation in English*. Mswada bado haujachapishwa. Nairobi.

Mutiso, K. (2004). al-Busiri and Muhammad Mshela: Two great sufi poets. *Swahili Forum*, (11), 83-90.

Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa hamziyyah*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Schimmel, A. (1975). *Mystical dimensions of Islam*. Chapel Hill: The University of North Carolina Press.

Schimmel, A. (1982). *As through a veil: Mystical poetry in Islam*. New York: Columbia University Press.

Schmid, W. (2013). http://www.lhn.uni-hamburg.de/node/63/revisions/232/view Ilisomwa 10 Juni 2017.

Shitemi, N. L. (2010). *Mashairi ya kabla ya karne ya ishirini*. Eldoret: Moi University Press.

Sufism (2017). Writings on Sufism. Imechukuliwa http://sufism.org/writingsonsufism Ilisomwa 26 Machi 2017

Taymiyah, A.A.A. (2000). *Ibn Taymiyah expounds on Islam: Selected writings of Shaykh al Islam Taqi ad din Ibn Taymiyyah on Islamic faith, life, and society. Compiled and translated by Muhammad Abdul Haqq Ansari.* Pdf

Wesah, W. E. (2005). *Uhakiki wa kifani katika utenzi wa Siri li Asirali* [afuan] *na utenzi wa Mwana Fatuma*.Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.



***Cite this article:***

Karama, M., Chimerah, R., na wa Mutiso, K. (2017). Ushairi wa Kisufi Katika Tendi za Kale za Kiswahili: Mfano wa Utendi wa Siri Li Asrari. *Mara res. j. Kiswahili*. Vol. 3, No. 1, Pages 1 - 9, ISSN 2520-0577